

### Taarifa kwa Vyombo vyta

**Tunaionya Japan Itahadhari na Matokeo ya Kuiunga mkono Serikali ya Wauaji ya Myanmar katika Mauaji yao ya Halaiki ya Warohingya, kwa kuwa Khilafah ya Uongofu inayokaribia kwa hakika italishughulikia suala hili kwa umakinifu**

Japan imeifuata India, kibaraka mwagine wa washambuliaji wa Kimagharibi, kwa kuiunga mkono serikali ya Myanmar kuhusiana na Mauaji ya halaiki ya Waislamu Warohingya. Balozi wa Japan nchini Myanmar, Ichiro Maruyama, bila aibu alisema siku chache zilizopita katika mukutano na waandishi wa habari kuwa hakukuwa na mauaji ya halaiki nchini Myanmar, badala yake ni ‘msako wa kupambana na ugaidi’ dhidi ya shirika la Kijihad la ‘Arakan Rohingya Salvation Army’ (Reuters, Januari, 15, 2020)! Hesabu za kutisha za kuenea ubakaji, mauaji ya watu wengi na kuviteketeza vijiji vyote, na ukimbizi wa Warohingya 740,000 ndani ya Bangladesh yote yametupiliwa mbali na Japan kwa sababu ya njama za kupambana na ugaidi zinazopigiwa debe ulimwenguni na Masalabiyyina wa Kimagharibi. Kwa kweli, msimamo rasmi wa Japan kuhusiana na mauaji ya halaiki ya Warohingya sio ‘kupinga’ hasa, badala yake ‘wanaidhinisha’ mauaji ya jumla ya Waislamu Warohingya ili kuingiliana na ‘vita dhidi ya Uislamu’ vinavyoongozwa na Amerika. Inasikitisha sana kuwa Japan imesahau uhusiano wa karibu iliyokuwa nao na Khilafah ya Uthmaniya wakati wa Sultan Abdul Hamid Khan na mfalme wao maarufu Meiji aliyebadilisha Japan kutoka jimbo la kujitenga na kuwa nguvu ya kiviwanda ulimwenguni. Tofauti na Mtawala Meiji aliyekuwa kiongozi mwenye maono na mwenye shauku kubwa juu ya Uislamu, tangu kushindwa Japan na Amerika, watawala watiifu wa Japan wamekuwa wakiishusha nchi yao kwa kufuata kiupofu njia ya uongo na udanganyifu mkubwa ya Amerika. Kwa hivyo, tumewaona wao wakipeleka majeshi yao kwenye vita vya Amerika kwenda Afghanistan ambavyo msingi wake ni uongo. Na sasa, twaiona serikali ya Japan bila aibu inahalalisha mauaji ya Waislamu kwa kisingizio cha kupigana na kinachojudikana kama ‘Ugaidi wa Kiislamu’.

**Hizb ut Tahrir / Wilayah Bangladesh**, inataka kutuma ujumbe mkali kwa Japan kuwa haifai kuunga mkono ukatili dhidi ya Waislamu Warohingya. Hata ingawa kwa sasa ni madhaifu na wanakandamizwa kwa sababu ya usaliti na kutokuwa na uwezo kwa watawala wa serikali ya taifa letu, udhaifu huu utamalizika kama mlezi na mlinzi wao wa kweli, Khilafah ya Uongofu ya pili kwa njia ya Utume, inakaribia kusimamishwa tena kwa matakwa yake Mwenyezi Mungu (swt) karibuni. Dola ya Khilafah inayokaribia hakika itaishughulikia ipasavyo Myanmar kwa dhuluma ambazo inawafanya Ummah wetu mpendwa, na pia itazihesabu zile nchi ambazo ziliunga mkono nchi hii yenyе vita vya chuki. Mjumbe wa Mwenyezi Mungu rehma na amani zimshukie alisema:

«إِنَّمَا إِلَامَ جُنَاحٌ يُقَاتَلُ مِنْ وَرَاهِهِ وَيَنْتَقِي بِهِ»

**“Hakika Imamu ni ngao watu hupigana nyuma yake na hutaka hifadhi kwake.”** [Muslim]

**Afisi ya Habari ya Hizb ut Tahrir  
Wilayah Bangladesh**

**Tovuti Rasmi ya Hizb ut Tahrir:**  
[www.hizb-ut-tahrir.org](http://www.hizb-ut-tahrir.org)